



MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO


Na: 36. Msimu wa Kilimo 2018/19 Tathmini Septemba 11-20, 2019 na Matazamio kwa Kipindi cha Septemba 21-30, 2019

Muhtasari

- Wakulima katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka wanashauriwa kuendelea na uandaaji wa mashamba kwa ajili ya msimu wa mvua za vuli unaotarajiwa.
- Hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua itasababisha upungufu wa maji na malisho kwa mifugo, hivyo wafugaji wanashauriwa kuzingatia matumizi endelevu ya maji na malisho

MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 11-20, 2019

Katika kipindi cha dikadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo eneo la kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika zaidi kulinganisha na ile iliyopo eneo la kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) ambayo iliendelea kupungua nguvu. Hali hii iliendelea kuuweka ukanda wima wa mvua magharibi mwa mwa nchi pamoja na ziwa Viktoria, ilihali ukisababisha mvua na ngurumo katika maeneo machache. Joto la juu kidogo ya wastani kusini magharibi mwa bahari ya Hindi liliendelea kusababisha kuimarika kwa mgandamizo mdogo wa hewa katika eneo hili na kupelekea pepo zenye unyevu kuvuma kuelekea pwani ya kaskazini mwa nchi yetu ikiambatana na mvua nyepesi. Hata hivyo, joto la juu kidogo ya wastani katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (Pwani ya Angola) liliendelea kudhoofisha kasi ya pepo za magharibi kuvuma kuelekea maeneo ya magharibi mwa nchi yetu.



Kielelezo 1: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Septemba 11- 20, 2019.

MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 11-20, 2019

Kwa kipindi hicho cha dikadi maeneo mengi ya nchi yalikuwa makavu isipokua kwa baadhi ya maeneo machache ya ukanda wa Ziwa Viktoria hususan magharibi, kusini na mashariki mwa ziwa Viktoria, mashariki na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma ambayo yamepata vipindi vichache vya mvua. Kiasi cha mvua kilichopimwa ni kati ya milimita 11 hadi milimita 50 inavyoonekana, kama inavyojieleza katika kielelezo.

TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 11-20, 2019

Katika kipindi cha dekadi iliyopita wakulima katika maeneo mengi yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka waliendelea na uandaaji wa mashamba isipokuwa katika mkoa wa Kagera ambapo wameanza kupanda mazao ya mahindi na maharage. Kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua wakulima wanaendelea na maandalizi ya mashamba kwa msimu wa kilimo unaotarajiwa kuanza mwezi Novemba au Disemba. Upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo ulikuwa wa wastani katika maeneo mengi ya nchi, isipokuwa katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Mwanza,

Mara, Simiyu, Shinyanga, Singida, Arusha, Manyara na Dodoma ambako hali ya maji na malisho iliendelea kupungua kuliko maeneo mengine ya nchi.

HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 11-20, 2019

Kina cha maji kwenye mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vililendelea kupungua kiasi kutokana na hali ya ukavu inayoendelea katika maeneo mengi ya nchi.

MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 21-30, 2019

Katika siku kumi zijazo za mwezi Septemba, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo eneo la kusini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kupungua nguvu katika nusu ya kwanza ya kipindi hiki ikilinganishwa na ile iliyopo eneo la kaskazini mwa dunia ambayo inatarajiwa kuimarika. Hali hii inatarajiwa kuendelea kuusogeza ukanda wima wa mvua maeneo ya yanayozunguka ukanda wa Ziwa Viktoria. Hata hivyo, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo eneo la kusini mwa dunia inatarajiwa kuimarika katika nusu ya mwisho ya kipindi hiki na kupelekea mkondo wa mgandamizo mkubwa wa hewa kusababisha upepo mkali maeneo ya ukanda wote wa pwani. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi. Hali hii inatarajiwa kuendelea kusababisha mvua nyepesi katika maeneo ya ukanda wa pwani ya kaskazini hususan nusu ya pili ya kipindi hiki. Aidha, joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika maeneo ya pwani ya Angola.

HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 21-30, 2019

KWa upande wa maeneo ya kanda ya Ziwa Viktoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) kunatarajiwa kuwa na vipindi vifupi vya mvua na ngurumo hususan katika maeneo ya magharibi mwa ukanda wa Ziwa Viktoria.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na

Kilimanjaro) kunatarajiwa kuwa na mawingu kiasi na mvua nyepesi hususan kuelekea mwishoni mwa kipindi hiki.

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) kunatarajiwa kuwa na vipindi vifupi vya mvua katika maeneo machache hususani nusu ya pili ya kipindi hiki.

Magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), Kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), Pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) na kanda ya kusini (mikoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) kunatarajiwa kuwa na mawingu kiasi na makavu kwa ujumla.

MATARAJIO NA USHAURI WA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 21-30, 2019

Hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka itapelekea kuendelea kupungua kwa maji ya mifugo na matumizi ya binadamu. Mvua zinazotarajiwa zitakua na manufaa kwa shughuli za uandaaji wa mashamba katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Wakulima, wavuvi na wafugaji wanashauriwa kufuata ushauri unaotolewa na maafisa ugani ili kunufaika na utabiri na ushauri huu.

HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 21-30, 2019

Kina cha maji kwenye mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kupungua kwa maeneo mengi ya nchi kutokana na hali ya ukavu inayoendelea. Watumiaji wa maji wanashauriwa kuwa na matumizi endelevu ya maji hususan maeneo ambayo yanatarajiwa kuwa na upungufu wa maji.

Jarida limetayarishwa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3-Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania